**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

*Zanzibar*
*08 Januari, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

## TAARIFA KWA UMMA

## KANUSHO KUHUSU TAARIFA ZA UTEUZI WA BI. CATHERINE WENCELAUS MOSHI KUWA BALOZI

Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu, inakanusha taarifa ya uongo inayosambaa mtandaoni kuhusu uteuzi wa Bi. **Catherine Wencelaus Moshi** kuwa Balozi. Taarifa hiyo si ya kweli na haijatolewa na Ikulu.

Upotoshaji huu umefanyika kutoka katika taarifa sahihi rasmi ya tarehe 08 Januari, 2026 iliyohusu uteuzi wa Mhandisi **Zena Ahmed Said** kuwa Balozi.

Kurugenzi inatahadharisha kuwa usambazaji wa taarifa hiyo ni upotoshaji, ambao ni kinyume cha sheria. Aidha, Kurugenzi inatoa wito kwa umma kuthibitisha taarifa zote rasmi za Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu kupitia vyanzo rasmi vya taarifa, ambavyo ni:

- **Kurasa za Instagram & Facebook:** Ikulu Tanzania @ikulu_mawasiliano;
- **Ukurasa wa X (Twitter):** ikulu_Tanzania @ikulumawasliano; na
- **Tovuti:** www.ikulu.go.tz.

Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu